TANGAZO LA SERIKALI NA. 379 la tarehe 15/5/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA. 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MINADA YA MIFUGO (MAREKEBISHO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2020

Jina

Tangazo la Serikali Na 96 la Mwaka 2011

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Minada ya Mifugo (Marekebisho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2020 na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ushuru wa Minada ya Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2011 ambayo katika Sheria Ndogo hii itajulikana kama “Sheria Ndogo Kuu”

Marekebisho ya kifungu cha 11

2. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha 11 na badala yake kuweka kifungu kipya kama kifuatacho:

> “11. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja”.

Marekebisho ya Jedwali la Tatu

3. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta Jedwali la Tatu na kuweka Jedwali jipya kama ifuatavyo:.

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 7)*

USHURU WA MINADA KWA MIFUGO INAYOUZWA

| Na. | Aina ya Mifugo | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 5,000/= kwa kila atakayeuzwa |
| 2. | Mbuzi, kondoo | 1,500/= kwa kila atakayeuzwa |
| 3. | Punda | 2,000/= kwa kila atakayeuzwa |
| 4. | Nguruwe | 2,000/= kwa kila atakayeuzwa |
| 5. | Kuku, bata, sungura | 500/= kwa kila atakayeuzwa |
| 6. | Mifugo mingine ambayo haikutajwa | 500/= kwa kila atakayeuzwa |

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Same umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na mkutano wa baraza la Madiwani Halmashauri ulioitishwa tarehe 15/3/2018.

ANNA CLAIRE SHIJA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

CHRISTOPHER M. IRIRA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,Same*

NAKUBALI,

L.S

*Dodoma,*
16 Aprili, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN OR-TAMISEMI*
*Dodoma*